**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 20 Mei, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa Mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa Mwaka 2021/2022.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango

96. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    (a) Je, kuna mpango wowote wa wanachama wa ZSSF kukopeshwa fedha kabla ya kufikia umri wao wa kustaafu.

    (b) Kama upo mpango huo, Je, utaratibu wa kukopa fedha hizo ukoje na vipi wanachama hao wanarejeshewa fedha zao.

### Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

12. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Kwa kuwa zaidi ya asilimia 50 ya Wazanzibari wamewekeza maisha yao katika kilimo, na kwa kuwa mazao mengi ya kilimo hukabiliwa na changamoto ya soko pale uzalishaji unapokuwa mkubwa jambo linaloathiri maisha ya wakulima wengi hususan wakulima wa nyanya, embe na mboga mboga.

    (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maisha ya wakulima hawa.

    (b) Ni lini Serikali italeta mpango wa kuifanya bei ya mazao hayo kuwa imara (Stable).

### Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

78. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

    Kwa muda mrefu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa na utamaduni wa kusamehe kodi kwa bidhaa muhimu wakati wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani ili kuleta unafuu kwa wananchi katika mwezi huu muhimu. Hata hivyo, tafiti zilizofanyika zinaonyesha kwamba wafanyabiashara hawa wanaopata unafuu wa kodi, huwa hawapunguzi bei za bidhaa zao, hali inayowaumiza wananchi na kuipunguzia Serikali mapato.

(a) Kwa kuwa hali hiyo inajitokeza kila mwaka na kwa kuwa wafanyabiashara wote wanaopata msamaha huu wanajulikana. Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na tatizo hili.

(b) Ni kiasi gani cha fedha ambacho Serikali ilisamehe kutokana na msamaha huo mwaka 2019/2020.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

26. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ni chuo kinachomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kilichokusudiwa kutowa taaluma ya Vitivo mbali mbali katika visiwa vyote viwili vya Zanzibar. Kwa kuwa eneo la Chamanagwe liliopo Mchangamdogo Pemba ni eneo zuri kwa ajili ya kilimo na mifugo.

Je, ni lini Serikali itaanzisha Kitivo cha Kilimo, tawi la Pemba (Faculty of Agriculture Pemba Branch) katika eneo la Chamanagwe.

117. MHESHIMIWA SULUBU KIDONGO AMOUR (Jimbo la Mkwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa katika skuli ya Mkwajuni kuna vijana wengi wazalendo waliojitolea kusomesha kwa muda mrefu sasa bila ya kuajiriwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaajiri vijana hao.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

32. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Tangi la Kironjo liliopo ndani ya Jimbo la Wingwi ni la miaka mingi sana.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulifanyia ukarabati.

(b) Kwa kuwa tangi hili limeshazidiwa na watumiaji, kwa nini Serikali isijenge tangi jengine kubwa na la kisasa ili kuweza kuwahudumia wananchi wote kwa urahisi.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

9. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kumekuwa na jitihada kubwa za Serikali katika kuinua sekta ya michezo kwa nchi yetu. Pamoja na jitihada hizo bado kuna uzito mkubwa kwa Serikali kufanya maamuzi ya kuiruhusu baadhi ya michezo. Kwa kuzingatia kuwa michezo ni afya, michezo ni ajira na ikitumika vizuri inaweza kuutangaza utalii wetu. Kwa vile Tanganyika na Zanzibar ni nchi mbili zilizoungana na kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zinazoipa ugumu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara husika kuruhusiwa mchezo wa ngumi (Boxing) pamoja na mchezo wa “kick- boxing” ili kuongeza ajira pamoja na kukuza na kuutangaza utalii wetu kupitia mabondia.

(b) Ni lini Serikali itaruhusu rasmi kuanza kwa mchezo huo hapa nchini.

**<u>Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>**

33. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Mbali na juhudi kubwa zinazochukuliwa na Serikali za kupambana na makosa mbali mbali bado matukio hayo yanaendelea kuripotiwa, ikiwa ni pamoja na makosa ya kuwatupa chooni, majaani na sehemu nyenginezo watoto wachanga wanaozaliwa.

(a) Je, ni watu wangapi wametuhumiwa kwa makosa ya kuvitupa vitoto vichanga visivyo na hatia kwa kipindi cha 2020/2021.

(b) Je, ni wangapi kati ya hao wamehukumiwa na ni adhabu gani walizopewa kwa makosa ya aina hii.

(c) Ni Wilaya gani inayoongoza ndani ya Zanzibar kwa matukio haya.

**IV. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>**

**<u>Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2021/2022.

**<u>Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**20 Mei, 2021.** **<u>KATIBU WA BARAZA</u>**